JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

# K I Z I D U O

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI CHA TAREHE 13/10/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI**

**A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA;**

1. Ndg. Denis kabogo - Kaimu Mkurugenzi (W) -Mwenyekiti
2. Ndg Angela Mulisa - kaimu Afisa Utumishi na Utawala (W) - Katibu
3. Ndg. Maro Christopher - Mkaguzi wa Ndani (W) - Mjumbe
4. Ndg. Peter Revelian - Mweka Hazina (W) - Mjumbe
5. Ndg. Pharles Mahushi - Afisa Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji(W) - Mjumbe
6. Ndg. Paulo J. Dotto - Kaimu Mwanasheria wa Halmashauri - Mjumbe
7. Ndg. Serapion Rujuguru - Afisa Mifugo na Uvuvi (W) - Mjumbe
8. Ndg. Nesphory Biswelo - Kaimu Afisa Usafishaji na Mazingira (W) - Mjumbe
9. Eng. Magreth Kavalo - Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika W) - Mjumbe
10. Dr. Elias Misana - Mganga Mkuu (W) - Mjumbe
2. Ndg. Vedastus Nyambalya - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) - Mjumbe
3. Ndg. William Kasuja - Kaimu Afisa TEHAMA - Mjumbe
4. Ndg. Rosalia Magotti - Afisa Maendeleo ya Jamii (W) - Mjumbe
5. Ndg. Wickriph Benda - Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) - Mjumbe
6. Ndg. Kulwa John - Afisa Manunuzi na Ugavi - Mjumbe
7. Ndg. Greyson Vuri - Kaimu Afisa Nyuki (W) - Mjumbe
8. Ndg. Beater Bwire - Kaimu Mtendaji Mamlaka M/mdogo Ngudu - Mjumbe
9. Ndg. Selestina Mushi - Mratibu wa TASAF - Mjumbe
10. Eng. John Msonga - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) - Mjumbe
11. Ndg. Wivina Byabato - Mratibu wa UKIMWI wa Halmashauri - Mjumbe
12. Ndg. Naitu Shawarija - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) - Mjumbe
13. Ndg. Kassimu Shomvi - Mhasibu wa matumizi - Mjumbe
14. Ndg. Mgisha Kaswa - Mhasibu wa mapato - Mjumbe

**B. SEKRETARIETI**

1. Ndg. Edmund M.Alois - Mwandishi wa Vikao
2. Ndg. Rahel A. Mdachi - Mwandishi wa Vikao
3. Ndg. Israel S. Petro - Mratibu wa Vikao

**AJENDA NA KDC/FUM/ . 21/10/2021/2022**

KDC/FUM/AJENDA NA. 21/10/2021/2022 – Kufungua Kikao
KDC/FUM/AJENDA NA. 22/10/2021/2022 – Kuthibitisha Ajenda
KDC/FUM/AJENDA NA. 26/10/2021/2022 – Taarifa ya mapokezi ya Fedha za Miradi kiasi cha Tsh. 3,411,782,615.69
KDC/FUM/AJENDA NA. 29/10/2021/2022 – Kufunga kikao.

**KDC/FUM/AJENDA NA. 21/10/2021/2022 - KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ambaye alifungua Kikao saa 4.00 Asubuhi.



Mtaa wa Kakora, S.L.P 88, Ngudu, SIMU : +255 (028) 2983121, Nukushi: +255 (028) 2983119 Barua Pepe: ded@kwimbadc.go.tz, dhro@kwimbadc.go.tz Tovuti: www.kwimbadc.go.tz

**KDC/FUM/AJENDA NA. 22/10/2021/2022 – KUTHIBITISHA AJENDA**
Ajenda ya Kikao zilithibitishwa na Wajumbe.

**KDC/FUM/AJENDA NA. 26/10/2021/2022 – TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI KIASI CHA TSH. 3,411,782,615.69**

Taarifa iliwasilishwa na Mweka Hazina (W) ambapo alieleza kuwa katika Mwezi Oktoba 2021 Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imepokea kiasi cha Tsh. 3,411,782,615.69 kwa ajili ya miradi mbalimbali kama ifuatavyo;

- Ujenzi wa madarasa 109 Elimu Sekondari Tzs 2,180,000,000.00
- Ujenzi wa Kituo cha Afya isunga Tzs 250,000,000.00
- Madeni ya Wazabuni na chakula mashuleni Tzs 113,586,995.69
- Mitihani Darasa la 4 Tzs 243,996,120.00
- Mitihani Darasa la 7 Tzs 229,954,500.00
- Mitihani Kdato cha 2 Tzs 149,142,500.00
- Mitihani Kdato cha 4 Tzs 245,102,500.00

**JUMLA KUU TSH. 3, 411,782,615. 69**

Pia alieleza kati ya fedha hizo kiasi cha Tsh. 2.180,000,000.00 ni kwa ajili ya madarasa 109 katika Shule za Sekondari ambapo madarasa hayo yanatakiwa yakamilike ifikapo tarehe 15/12/2021 kulingana na maelekezo ili wanafunzi wapate vyumba vya kusome pindi shule zitakapo funguliwa Januari 2022.

Aidha. ,aliwajulisha wajumbe kuwa Halmashauri imepokea fedha nyingine kiasi cha Tzs 75,000,000.00 zilizo tumwa katikati ya mwezi Septemba 2021 kwaajili ya ukamilishaji wa Madarasa katika shule tatu (3) ambazo ni;

(I) Nyamigamba Sekondari Madarasa 2 kwa kiasi cha fedha Tzs 25,000,000.00
(II) Mwashilalage Sekondari Madarasa 2 kwa kiasi cha fedha Tzs 25,000,000.00 na
(III) Hungumalwa Sekondari Madarasa 2 kwa kiasi cha fedha Tzs 25,000,000.00

Baada ya Wajumbe kupitia taarifa hiyo waliipokea walishauri kama ifuatavyo;-
wajumbe waliipongeza na kuishukuru Serikali kwa kuleta fedha za ukamilishaji wa madarasa hayo na itawarahisishia wananchi kupata madarasa ya watoto kujifunzia. Walikubaliana waweke usimamizi mzuri katika matumizi ya fedha hizo zilizoletwa ili madarasa hayo yakamilike mapema na mwezi Januari 2022 wanafunzi wayatumie.
Mjumbe alishauri walezi wa kata wote na Menejimenti washiriki kikamilifu kusimamia miradi hiyo kila anayehusika ahakikishe madarasa yanakamilika kwa wakati

Mjumbe alisema fedha hizi zimekuja na maelekezo hivyo kila mmoja ayaelewe vizuri maelekezo hayo ili kazi ikamilike kwa ubora na kwakufuata maelekezo ya Serikali
Wajumbe walikubaliana manunuzi ya bidhaa za viwandani yafanyike kwa pamoja ili kupunguza gharama na kurahisisha ufuatiliaji madokezo ya manunuzi yavifaa vya viwandani yaanzishwe haraka malighafi za ujenzi kama mchanga kokoto mawe yanunuliwe na kukusanywa kutoka kwenye maeneo ya karibu na mradi ili kupunguza gharama. Wazabuni watakaoleta tofari watafutwe haraka na mikataba ifungwe ili kazi zianze Taarifa ya utekelezaji wa miradi hii itolewe kwa maandishi kila jumatatu ili menejimenti iwe na uelewa wa pamoja utakaosaidia kufanya ufuatiliaji

**KDC/FUM/AJENDA NA. 29/10/2021/2022 – KUFUNGA KIKAO.**
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ambaye alifunga Kikao saa 8.10 Mchana.

| | | |
|---|---|---|
| | **UMETHIBITISHWA.** | |
| .............................. | 26.10.2021 .............................. | .............................. |
| **MWENYEKITI** | | **KATIBU** |



Mtaa wa Kakora, S.L.P 88, Ngudu, SIMU : +255 (028) 2983121, Nukushi: +255 (028) 2983119 Barua Pepe: ded@kwimbadc.go.tz ,dhro@kwimbadc.go.tz , Tovuti: www.kwimbadc.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

**KIZIDUO**
**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA MENEJIMENTI YA HALMASHAURI CHA TAREHE11/01/2022**

### A. WATAALAM WALIOHUDHURIA;

1. Ndg. Happiness Msanga - Mkurugenzi Mtendaji (W) -Mwenyekiti
2. Ndg. Israel Petro - Kaimu Afisa Utumishi (W) - Katibu
3. Ndg. Christopher Maro - Mkaguzi wa Ndani (W) - Mjumbe
4. Ndg. Peter Revellian - Mweka Hazina (W) - Mjumbe
5. Ndg. Yohana Mhandikila - Kny. Afisa Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji(W) -Mjumbe
6. Ndg. Paulo Dotto - Kaimu Mwanasheria (W) - Mjumbe
7. Ndg. Emmanuel Katemi - Kaimu Afisa Elimu Sekondari (W) - Mjumbe
8. Ndg. Serapion Rujunguru - Afisa Mifugo na Uvuvi (W) - Mjumbe
9. Ndg. Nesphory Biswalo - Kaimu Afisa Usafishaji na Mazingira (W) - Mjumbe
10. Eng. Magreth Kavalo - Afisa Kilimo,Umwagiliaji na Ushirika W - Mjumbe
11. Dr. Elias Misana - Mganga Mkuu (W) -Mjumbe
12. Ndg. Vedastus Nyambalya - Kaimu Afisa Elimu Msingi (W) - Mjumbe
13. Ndg. Wivina yabyato - KaimuAfisa Maendeleo ya Jamii (W) - Mjumbe
14. Ndg. Joshua Majimbe - Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) - Mjumbe
15. Ndg. Denis Kabogo - Afisa Uchaguzi (W) - Mjumbe
16. Ndg. Greyson Vuri - Kaimu Afisa Nyuki (W) - Mjumbe
17. Eng. John Msonga - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W) - Mjumbe
18. Ndg. Kassim Shomvi - Mhasibu wa Matumizi - Mjumbe
19. Ndg. Beater Bwire - Kaimu Mtendaji Mamlaka M/mdogo Ngudu - Mjumbe
20. Ndg. Fortunata Mpuya - Afisa Mipango - Mjumbe
21. Ndg. Mbaraka Kaombwe - Afisa Mipango - Mjumbe
22. Ndg. Clavery Reginald - Afisa Utumishi - Mjumbe

### B. WAKARIBISHWA

Hakuna

### C. SEKRETARIETI

1. Ndg. Rahel A. Mdachi - Mwandishi wa Vikao
2. Ndg. Edmund M. Alois - Mwandishi wa Vikao
3. Ndg. Israel s. Petro - Mratibu wa Vikao



Mtaa wa Kakora, S.L.P 88, Ngudu, SIMU : +255 (028) 2983121, Nukushi: +255 (028) 2983119
Barua Pepe: ded@kwimbadc.go.tz ,dhro@kwimbadc.go.tz , Tovuti: www.kwimbadc.go.tz

**AJENDA NA.07/01/2021/2022**

**DONDOO ZA KIKAO**

1. Agenda Na. 57/01/2021/2022 - Kufungua kikao.
2. Agenda Na. 58/01/2021/2022 - Kuthibitisha ajenda.
3. Agenda Na. 65/01/2021/2022 - Taarifa ya ujenzi wa jengo la dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya eneo la icheja na Nyumba ya mtumishi katika Zahanati ya Shushi
4. Agenda Na. 67/01/2021/2022 –Kufunga kikao.

**KDC/CMT/AJENDA NA. 57/01/2021/2022 – KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwaeleza wajumbe hiki ni kikao cha robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kitakachojadili ajenda zote zilizoorozeshwa hapo juu. kisha alimkaribisha Mwenyekiti ambaye alifungua kikao saa 2:50 Asubuhi.

**KDC/CMT/AJENDA NA. 58/01/2021/2022 – KUTHIBITISHA AJENDA**

Katibu aliwaongoza wajumbe kupitia ajenda 11 zilizowasilishwa mbele ya wajumbe na wajumbe wote kwa pamoja walizithibitisha ili zijadiliwe ikiwemo ajenda ya . Taarifa ya ujenzi wa jengo la Dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya eneo la Icheja na Nyumba ya mtumishi katika zahanati ya shushi

**KDC/FUM/ AJENDA NA 65/02/2021/2022-TAARIFA YA UJENZI WA JENGO LA DHARULA (EMD) KATIKA HOSPITALI YA WILAYA ENEO LA ICHEJA NA NYUMBA YA MTUMISHI KATIKA ZAHANATI YA SHUSHI**

Taarifa iliwasilishwa na Mwekahazina wilaya akieleza kuwa Halmashauri imepokea fedha sh 90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi ( 3 in one) katika zahanati ya Shushi, Pamoja na sh 300,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la dharura katika Hospitali ya Wilaya Eneo la Icheja. Fedha hizi zilikuja na maelekezo kutoka Serikali kuu kwamba watumie wakandarasi katika utekelezaji wa miradi hiyo

Wajumbe wa Menejimenti ya Halmashauri walikubaliana mchakato wa kuwapata wakandarasi uanze haraka ikiwa ni pamoja na kuweka tangazo la zabuni ya kazi ya ujenzi ili wenye sifa waombe zabuni hiyo.Aidha wajumbe walimtaka mhandisi wa ujenzi aandae BOQ za majengo hayo kwa kuzingatia bei halisi na apewe Afisa maunuzi kwa ajili ya utekelezaji.

Wajumbe waliridhia ujenzi wa jengo la dharura (EMD) katika Hospitali ya Wilaya eneo la Icheja na Nyumba ya Mtumishi katika Zahanati ya Shushi utekelezaji uanze maramoja.ili kuendana na maelekezo ya Serikali.

**KDC/CMT/AJENDA NA. 66/01/2021/2022 – KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao kisha alifunga kikao saa 12:30 Jioni.

**UMETHIBITISHWA.**

| | | |
|---|---|---|
| [signature] | 03.02.2022 | [signature] |
| **MWENYEKITI** | **TAREHE** | **KATIBU** |



Mtaa wa Kakora, S.L.P 88, Ngudu, SIMU : +255 (028) 2983121, Nukushi: +255 (028) 2983119
Barua Pepe: ded@kwimbadc.go.tz ,dhro@kwimbadc.go.tz , Tovuti: www.kwimbadc.go.tz